PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA

PPAA
Toleo Na: 08 Januari - Machi 2026

# BULLETIN

"UTATUZI WA MIGOGORO KWA HAKI NA WAKATI"



*Katibu Mtendaji - PPAA*
*Bw. James Sando*

## PPAA yawanoa wazabuni 1,296 matumizi ya Moduli

**MPENDWA msomaji wa Jarida la "PPAA Bulletin" karibu tena ujisomee Toleo la Nane (08) la Jarida la Mtandaoni kutoka Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA). Jarida hili ni moja kati ya njia inazozitumia PPAA katika mawasiliano yake ya kimkakati ya kuwahabarisha wadau wa ununuzi wa umma na umma kwa ujumla kuhusu shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi mitatu.**

Ninayo furaha kukuletea Toleo la Nane la PPAA Bulletin kwa kipindi kingine tena cha miezi mitatu (Januari – Machi, 2026), kwa lengo la kukuhabarisha shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi hicho.

Mbali na kutekeleza jukumu lake la msingi la sekta ya ununuzi wa umma kushughulikia malalamiko na rufaa zilizowasilishwa mbele yake kwa kipindi tajwa, PPAA imefanikiwa kuwajengea uwezo wazabuni 1,296 na makundi maalum juu ya uwasilishaji wa malalamiko na rufaa katika mfumo wa (NeST). Mafunzo haya yamewawezesha wazabuni kufahamu haki walizonazo katika michakato ya ununuzi wa umma. Mafunzo hayo yamefanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma,Mbeya, Mwanza, Ruvuma, Njombe, Iringa, Lindi, Mtwara na Wiliaya ya Kilwa.

Mikoa mingine ni Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe na Iringa pamoja na Wilaya ya Kilwa ambapo mafunzo katika mikoa na wilaya yamefanyika kati ya Januari – Machi, 2026.

Aidha, katika toleo hili, tumekuandalia habari mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya PPAA katika kufikia malengo iliyokusudia kwa kipindi tajwa.

Karibu usome jarida hili ili ufahamu kwa undani PPAA na shughuli ilizozitekeleza katika kipindi cha miezi mitatu (Januari – Machi, 2026) na kuendeleza ushirikiano imara katika utoaji rufaa kwa ufanisi, wakati na kwa haki kwenye sekta ya ununuzi wa umma.

***#Kazi na Utu, Tunasonga Mbele.***
***Karibu Sana***

# PPAA yatoa mafunzo kwa vijana 878

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imefanikiwa kuwajengea uwezo vijana 878 juu ya uwasilishaji wa malalamiko na rufaa katika mfumo wa (NeST). Mafunzo haya yamewawezesha vijana kufahamu haki walizonazo katika michakato ya ununuzi wa umma.**

"Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amebainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya taasisi hiyo na fursa kwa vijana Februari 25, 2026 katika ukumbi wa Idara ya Habari (MAELEZO) chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mtumba jijini Dodoma.

"Bw. Sando amesema mafunzo hayo yametolewa katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza na Mbeya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji

> Inaendelea ukurasa wa 2



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma - PPAA, Bw. James Sando (aliyekaa Katikati), Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Sheria - PPAA, Bi. Florida Mapunda (kushoto), Meneja wa Huduma za Taasisi – PPAA, Bw. Paschal Kajuna (kulia) pamoja na waandishi wa habari, wakiwa kaatika ukumbi wa Idara ya Habari (MAELEZO) katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mtumba jijini Dodoma wakisubiri kuuhabarisha umma mafanikio ya PPAA na fursa kwa vijana Februari, 2026.*

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 08 Januari - Machi 2026

# PPAA yatoa mafunzo kwa vijana 878

< Inatoka ukurasa wa 1

wa azma ya serikali ya kuwawezesha vijana na makundi maalumu kushiriki kikamilifu katika sekta ya ununuzi wa umma.

"Katika kipindi cha uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, PPAA imeendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia na kushughulikia rufaa zote zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma kwa misingi ya haki, uwazi na uadilifu.

"Bw. Sando ameongeza kuwa katika mashauri 196 yaliyosajiliwa na PPAA kwa kipindi cha uongozi wa Dkt. Samia, mamlaka hiyo imefanikiwa kuzuia utoaji wa tuzo za zabuni 43 za thamani ya TZS Bilioni 586. 5 kwa wazabuni waliokosa uwezo wa kifedha na sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika.

"Hatua ya Mamlaka ya Rufani (PPAA) kuzuia utoaji wa tuzo kwa wazabuni 43 waliokosa sifa za kutekeleza zabuni, inaimarisha mchakato wa usuluhishi wa migogoro ambayo ni moja ya falsafa nne za Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan," ameongeza Bw. Sando.

"Aidha Bw. Sando ameongeza kuwa PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), imekamilisha ujenzi wa Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

"Moduli hii ipo katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa Njia ya Kielektroniki (NeST) na inatoa njia rahisi, ya haraka na yenye uwazi kwa wadau wote kushiriki katika mchakato wa usulushi wa migogoro ya ununuzi hali inayochangia kwa kiasi kikubwa kuboresha utendaji na kuimarisha imani katika mfumo wa ununuzi wa umma," amesema Bw. Sando.

Matumizi ya Moduli yameleta mageuzi chanya katika namna taasisi za umma zinavyoshirikiana na PPAA kupokea, kusajili na kushughulikia malalamiko na rufaa kutoka kwa wazabuni walioshiriki katika michakato ya ununuzi wa umma.

"Hadi sasa, jumla ya malalamiko 549 yamewasilishwa na kushughulikiwa na taasisi nunuzi kupitia Moduli hiyo na rufaa 26 zimewasilishwa na kushughulikiwa na Mamlaka ya Rufani (PPAA) kupitia moduli,"




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akiwaeleza waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu mafanikio ya taasisi hiyo katika ukumbi wa Idara ya Habari (MAELEZO) chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mtumba jijini Dodoma, Februari, 2026.*

amebainisha Bw. Sando.

Matumizi ya moduli hiyo yameongeza ufanisi katika usimamizi wa rufaa, kupunguza muda wa kushughulikia mashauri na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa haki.

Kuanzishwa rasmi kwa matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kumeleta faida nyingi ikiwemo kuokoa muda katika mchakato wa kushughulikia malalamiko na rufaa na kupunguza gharama zinazohusiana na usuluhishi wa migogoro ya ununuzi.

Vilevile, moduli ya malalamiko na rufaa imewezesha kuongeza ufanisi wa utendaji wa taasisi zinazohusika, imehakikisha uwazi na uwajibikaji katika mchakato mzima wa ununuzi, imehifadhi kumbukumbu za malalamiko na rufaa kwa usahihi na urahisi wa kufuatilia pamoja na kuwezesha mzabuni kufuatilia hatua za rufaa yake pamoja na kupata nyaraka zote zinazohusiana kupitia mfumo wa NeST.

Bw. Sando amebainisha pia kuwa, PPAA imeendelea kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya Moduli ya kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST ambapo wazabuni 1,693 na watumishi 1,739 katika mwaka wa fedha 2025/26 wa ofisi mbalimbali za umma wamepatiwa mafunzo hayo.


BULLETIN
PPAA yawanoa wazabuni 1,296 matumizi ya Moduli
PPAA yatoa mafunzo kwa vijana 878

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Florida Mapunda

**Mhariri**
Gloria Tesha
Mwandishi wa TSN

**Wajumbe**
Agnes Sayi
Mohamed Makame
Humphrey Kisanga

**Katibu**
Nelson Kessy

**Mawasiliano:**
**Katibu Mtendaji**
5 Mkandarasi Place,
Ghorofa ya nne, 58
Barabara ya Lusinde,
S.L.P. 1385, 41104 Dodoma
Simu: +255 (0) 743505505,
Baruapepe: barua@ppaa.go.tz
es@ppaa.go.tz
Tovuti: www.ppaa.go.tz



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Bw. Denis Simba akifungua mafunzo ya siku moja kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST kwa wazabuni wa Mkoa wa Dar es Salaam yaliofanyika Januari 2026.*

# Wazabuni 2,000 wapigwa msasa matumizi ya NeST

## ■ Watakiwa kuzingatia sheria

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) zimeendesha mafunzo kwa wazabuni takribani 2,000 kuhusu Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa Njia ya Kielektroniki (NeST) katika mikoa minne tofauti.**

Wazabuni waliopatiwa mafunzo hayo wanatoka katika mikoa minne ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma na Mbeya ambapo pamoja na mambo mengine, mafunzo hayo yalijikita katika maeneo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 na kanuni zake, wajibu wa wazabuni katika ununuzi wa umma na uuzaji wa bidhaa kwa kutumia NeST.

Maeneo mengine ni majadiliano (negotiations) kwa kutumia mfumo wa NeST, kuwasilisha dhamana ya utekelezaji wa mkataba, kuomba malipo ya utekelezaji wa mkataba pamoja na uwasilishaji wa malalamiko na rufaa katika zabuni za umma.

Akifungua mafunzo hayo ya siku moja jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Bw. Denis Simba amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha wazabuni kuhusu mfumo wa NeST ili waweze kuondokana na changamoto zilizokuwa zinawakabili wakati wa kuomba zabuni za umma.

Aidha, Bw. Simba amesema kuwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2023 imeweka upendeleo maalum kwa wazabuni wa ndani ambapo miradi yote yenye thamani ya Shilingi bilioni 50 inatakiwa kutekelezwa na wazabuni Watanzania (wazawa).

"PPRA ina uhakika wa kusimamia vizuri sheria hii ya ununuzi wa umma na kuhakikisha kuwa mfumo huu wa NeST ili kuwapa fursa na kuwarahisishia kufanya kazi kwa haraka na wepesi zaidi........ kwa hiyo wazabuni nawasihi kutumia fursa ya mafunzo haya vyema ili kupata uelewa mpana wa mfumo huu wa NeST," amesema Bw. Simba.

Bw. Simba ameongeza kuwa mfumo wa NeST umeweka mazingira rafiki kwa wazabuni akisisitiza: "PPRA inatoa wito kwenu kutekeleza wajibu wenu kwa uadilifu, kuzingatia sheria na kanuni za ununuzi wa umma. Kwa kutumia mfumo, Mamlaka imeweza kuondoa janjajanja nyingi ambapo imesaidia serikali kupata thamani ya fedha katika miradi mbalimbali".

Aliongeza: "Nawasihi kuzingatia sheria, epukaneni na konakona nyingi zisizo na manufaa kwenu na ununuzi wa umma kwa ujumla, mfumo wetu kwa sasa umeunganishwa 'intergrated' na mifumo mingine kama vile Brela, Muce n.k. hivyo nawahakikishia kuwa hivi karibuni tutaondokana na changamoto ya ucheleweshaji wa malipo kwa wazabuni," amesema Bw. Simba.

Naye Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Huduma za Sheria wa PPAA, Bi. Florida Mapunda amesema lengo la mafunzo hayo ni kuwaelimisha wadau wa ununuzi wa umma kuhusu matumizi ya moduli ya usimamizi wa malalamiko na rufaa kielektroniki kwa mfumo wa NeST.

"Kwa sasa Sheria ya Ununuzi wa Umma imeweka sharti la lazima kwa ununuzi wa umma kufanyika kwa njia ya Kieletroniki kupitia mfumo wa NeST. Kutokana na sharti hilo, PPAA kwa kushirikiana na PPRA tumejenga moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST ili kuwasaidia wadau wa ununuzi kuwasilisha malalamiko na rufaa kieletroniki," amesema Bi. Mapunda.

Bi. Mapunda aliongeza kuwa, moduli imerahisisha zoezi la uwasilishaji wa malalamiko yatokanayo na michakato ya ununuzi wa umma pamoja na kusaidia utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za malalamiko na rufaa ambazo zitakuwa zinawasilishwa katika michakato yote ya ununuzi wa umma.

Mafunzo hayo ya siku moja kuhusu matumizi ya Mfumo wa NeST yamefanyika tarehe 10 Januari 2026 katika mikoa ya Dar es Salaam lengo likiwa ni kuendelea kutoe elimu kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma nchini.



*Sehemu ya wazabuni wa Mkoa wa Dar es Salaam wakifuatilia mafunzo kuhusu fursa za mfumo wa NeST yaliofanyika Januari, 2026.*

# Wazabuni na Taasisi Nunuzi za Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Njombe wajengewa uwezo matumizi moduli ya rufaa



*Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Florida Mapunda akiwasilisha mada kuhusu uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko katika mfumo wa NeST kwa wazabuni na taasisi nunuzi walioshiriki mafunzo mkoani Ruvuma hivi karibuni.*

**MAMLAKA ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imewakutanisha wazabuni na taasisi nunuzi wa mikoa ya Ruvuma, Iringa na Njombe na kuwajengea uwezo kuhusu Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa kwenye Mfumo wa NeST kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi.**

Mafunzo hayo yaliofanyika kwa nyakati tofauti katika miji ya Songea na Iringa hivi karibuni yamewahusisha washiriki 380 ambao ni wazabuni, wataalamu wa ununuzi, sheria, tehama na makundi maalumu yakiwemo wanawake, vijana, wazee na wenye mahitaji maalumu pamoja na mafundi wa ndani.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo, Katibu Mtendaji wa PPAA, Bw. James Sando amesema mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa na PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa lengo la kuwajengea uwezo wazabuni na taasisi nunuzi ili kuwapa ufanisi zaidi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao, hususan katika kushughulikia malalamiko na migogoro inayotokana na michakato ya ununuzi wa umma.

"Mafunzo haya yanalenga kuimarisha utendaji kazi wenu, kuhakikisha ufanisi, kuongeza uelewa wa matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa Njia ya Kielektroniki (NeST)," amesema Bw. Sando.

Bw. Sando ameongeza kuwa katika kutimiza azma ya serikali mafunzo yamewashirikisha vijana, wanawake na makundi maalumu ili kuwawezesha kupata elimu kuhusu ununuzi wa umma hususan katika michakato ya ununuzi na kuhakikisha wanaisaidia serikali kupata thamani halisi ya fedha katika miradi ya kimkakati yenye tija kwa taifa.

Pamoja na mambo mengine, Bw. Sando amewasihi washiriki kutumia mafunzo hayo kujifunza namna moduli ya kuwasilisha malalamiko na rufaa inavyofanya kazi katika Mfumo wa NeST kwani inatoa njia rahisi ya haraka na yenye uwazi kwa wadau wote kushiriki mchakato wa ushughulikiaji wa malalamiko yanayotokana na michakato ya zabuni za umma.

"Matumizi ya moduli yameongeza ufanisi katika usimamizi wa rufaa, kupunguza muda wa kushughulikia mashauri, na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa haki, kuokoa muda na kupunguza gharama zinazohusiana na usuluhishi wa migogoro ya ununuzi," ameongeza Bw. Sando.

Kwa upande wake Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Sheria wa PPAA), Bi. Florida Mapunda amesema mafunzo hayo yamelenga kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi wa umma kuhusu taratibu za uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST.

"PPAA kwa kushirikiana na PPRA tumejenga moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST ili kuwasaidia wadau wa ununuzi wa umma (wazabuni na taasisi za umma) kuwasilisha malalamiko na rufaa kwa ufanisi zaidi kupitia mtandao," amesema Bi. Mapunda.

Bi. Mapunda ameongeza kuwa tangu kuanza kwa matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST, takribani mashauri 596 yamewasilishwa kupitia mfumo huo, jambo linaloifanya PPAA kuendelea kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi wa umma ili waweze kufahamu namna sahihi ya matumizi ya moduli hiyo.

Kupitia mafunzo hayo, mada zilizowasilishwa ni pamoja na uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa katika ununuzi wa umma, uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko katika mfumo wa NeST, utoaji wa tuzo, uandaaji, upekuzi, na utiaji saini wa mkataba.

Mada nyingine zilizowasilishwa ni uwasilishaji na ushughulikiaji wa maombi ya kuongezewa muda wa kuwasilisha rufaa nje ya muda pamoja na uwasilishaji na ushughulikiaji wa rufaa katika mfumo wa NeST.

Mafunzo kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST yaligawanyika katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilifanyika Songea mkoani Ruvuma tarehe 02 na 03 Machi, 2026 na awamu ya pili ilifanyika Iringa mjini, kwa mikoa ya Iringa na Njombe tarehe 05 na 06 Machi, 2026.



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akifafanua jambo wakati ujumbe wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (RPPA) ya Rwanda ulipofanya ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu katika kushughulikia malalamiko na rufaa hususan kwa kutumia Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa iliyopo katika Mfumo wa NeST katika ofisi za PPAA jijini Dodoma Januari, 2026.*

# RPPA ya Rwanda yafanya ziara PPAA

**IKIWA ni udhihirisho wa hatua kubwa iliyopiga Tanzania katika mifumo, ujumbe wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (RPPA) ya Rwanda, umefanya ziara ya kujifunza na kubadilishana uzoefu katika sekta ya ununuzi wa umma nchini hususan Moduli ya Kupokea na Kushughulikia Malalamiko na Rufaa iliyopo katika mfumo wa NeST.**

Pamoja na mambo mengine, ziara hiyo imelenga kujifunza jinsi Mfumo wa NeST nchini Tanzania unavyofanya kazi katika kuhakikisha ununuzi wa umma unatekelezwa kwa uwazi, usawa na haki na kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha.

Akizungumza baada ya kuupokea ujumbe wa RPPA Januari mwaka huu, Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando amewahakikishia ushirikiano wakati wote wa ziara yao na kusema kuwa baada ya serikali kuelekeza matumizi rasmi ya mfumo wa NeST, PPAA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ilijenga moduli hiyo ya kuwasilisha malalamiko na rufaa.

Amesema lengo ni kutoa fursa zaidi kwa wazabuni kuwasilisha malalamiko na rufaa zao pindi wanapoona hawakutendewa haki katika michakato ya ununuzi wa umma.

"Manufaa ya kutumia moduli ni kwamba mzabuni anaweza kuwasilisha malalamiko/rufaa yake bila kufika ofisi za PPAA, inapunguza gharama na muda, pia mzabuni anaweza kuona rufaa yake imefikia hatua gani na nyaraka zote zinapatikana katika mfumo wa NeST, jambo linalochangia kuongeza uwazi zaidi," amesema Bw. Sando

Bw. Sando ameongeza kuwa, moduli hii imekuja baada ya PPAA kubaini mapungufu mbalimbali yaliyokuwa yanajitokeza wakati wa kusikiliza rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi wa umma ambapo zimekuwa zikiwasilishwa nje ya mfumo ya kidijitali ikiwemo, utunzaji hafifu wa kumbukumbu, gharama na ukosefu wa nyaraka kwa wakati.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa RPPA, Bw. Jimmy Byukusenge amesema wamekuwa wakifuatilia kwa karibu Mfumo wa ununuzi wa umma Tanzania na kugundua mfumo huo ni moja kati ya mifumo inayofanya vizuri katika ukanda wa Afrika Mashariki na ndiyo sababu ya ujumbe huo kuja kujifunza kutoka Tanzania ili kuwezesha Rwanda kusimamia ununuzi wa umma kwa uwazi, usawa na haki.

"Tumeamua kuja Tanzania kufanya ziara hii ili kujifunza namna Mfumo wa NeST unavyofanya kazi, pamoja na moduli zake, hususani hii ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa ili kutuwezesha na sisi Rwanda tuweze kuuboresha na kuutumia kama kigezo (benchmark) cha kufanya maboresho nchini kwetu," amesema Bw. Byukusenge.

Mbali na kufanya ziara PPAA, ujumbe huo pia umefanya ziara ya kujifunza katika ofisi za PPRA, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA).

Kikao cha ziara hiyo ya kujifunza kilihudhuriwa na Menejimenti ya PPAA na ujumbe wa RPPA uliongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Bw. Byukusenge aliyeambatana na Mtaalam Mwandamizi wa Ununuzi kutoka Tawi la Benki ya Dunia – Kigali, Bw. Sreenivas Devarakonda pamoja na Meneja Mradi wa Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki, Bi. Francine Gatarayiha.




*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando (aliyekaa katikati), Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (RPPA) ya Rwanda, Bw. Jimmy Byukusenge (wa pili kulia) wakiwa na baadhi ya watumishi wa PPAA na ujumbe kutoka RPPA baada ya kumaliza ziara ya kujifunza na kubadilisha uzoefu katika kushughulikia malalamiko na rufaa katika ofisi za PPAA Januari, 2026 jijini Dodoma.*

# Wadau wa ununuzi wa Njombe, Iringa waaswa kuzingatia maadili

**WADAU wa ununuzi katika mikoa ya Njombe na Iringa wameaswa kuzingatia maadili ya taaluma ya ununuzi wa umma pindi wanapotekeleza majukumu yao ili kuiwezesha serikali kupata thamani halisi ya fedha.**

Rai hiyo imetolewa na Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando alipokuwa akifunga mafunzo ya siku mbili kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo NeST kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kutoka taasisi za serikali kwa mikoa ya Njombe na Iringa yaliyofanyika tarehe 05 hadi 06 Machi, 2026 mjini Iringa.

Bw. Sando amesema baadhi ya kesi zinazowasilishwa PPAA kwa asilimia kubwa zinakuwa zimesababishwa na ukiukwaji wa maadili ya baadhi ya watumishi wasio waadilifu.

"Kama wadau katika sekta ya ununuzi wa umma ni muhimu kuzingatia maadili kwa sababu ndiyo itakayoipatia serikali thamani halisi ya fedha na heshima katika taaluma yenu, sote tunajua mifumo ya ununuzi ipo lakini inaongozwa na binadamu kama hawana maadili mifumo haiwezi kuisaidia Serikali," amesema Bw. Sando.

Kadhalika, Bw. Sando amewataka washiriki waliopata fursa ya kushiriki mafunzo hayo kuwaelimisha wadau wengine kuhusu matumizi ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST).



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando (aliyekaa katikati), Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Sheria wa PPAA, Bi. Florida Mapunda (aliyekaa kushoto) pamoja na Mkuu wa Sehemu ya Sheria wa PPAA, Bi. Agnes Sayi (aliyekaa kulia) baada ya kuhitimisha mafunzo ya siku mbili kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo NeST kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kutoka taasisi za serikali kwa mikoa ya Njombe na Iringa yaliyofanyika tarehe 05 hadi 06 Machi, 2026 mjini Iringa.*

Naye mdau wa ununuzi wa umma aliyeshiriki mafunzo hayo Bw. Danford Mfikwa aliipongeza PPAA kwa kuandaa mafunzo hayo ya siku mbili kwani yamewasaidia kufahamu namna ya kuwasilisha malalamiko na rufaa zitokanazo na michakato ya ununuzi kwa wakati kupitia moduli iliyopo katika mfumo wa NeST.

Mafunzo hayo ya siku mbili kwa mikoa ya Njombe na Iringa yamefanyika Iringa kuanzia tarehe 05 hadi 06 Machi, 2026 ambapo yamehudhuriwa na washiriki 240 kutoka mikoa hiyo.

Mafunzo hyo ni mwendelezo wa mafunzo yaliyofanyika Ruvuma tarehe 02 hadi 03 Machi, 2026, Kilwa tarehe 16 Februari, 2026 yakifuatiwa na ya Lindi na Mtwara tarehe 17 hadi 19 Februari, 2026.



*Sehemu ya washiriki wa mafunzo ya siku mbili kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo NeST kwa wazabuni na wadau wa ununuzi wa umma kutoka taasisi za serikali kwa mikoa ya Njombe na Iringa yaliyofanyika tarehe 05 hadi 06 Machi, 2026 mjini Iringa.*

# PPAA yatupilia mbali rufaa ya Kikundi cha Juhudi Mwenge Group dhidi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetupilia mbali rufaa iliyowasilishwa na Kikundi cha Juhudi Mwenge Group dhidi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).**

Rufaa hiyo ilitokana na uamuzi wa NHIF kuiondoa zabuni ya Mrufani kufuatia kushindwa kuthibitisha uwezo wake wa kifedha, ambapo wazabuni walitakiwa kuonyesha uwezo wa kupata rasilimali fedha zisizopungua Milioni Hamsini (TZS 50,000,000) ili kuhakikisha utekelezaji wa mkataba kwa ufanisi.

Mrufani alieleza kuwa alikidhi kigezo hicho kwa kuwasilisha barua iliyoainisha vyanzo vya fedha, akisisitiza kuwa hakukuwa na mwongozo maalum wa nyaraka zinazotakiwa. Pia barua hiyo ilibainisha kuwa ana akaunti kwenye benki ya DCB na NMB zinazomwezesha kupata mikopo, pamoja na kuonesha mapato ya fedha taslimu kutoka kwa wateja wake, hali inayoonyesha uwezo wa kufikia kiasi hicho tajwa.


Aidha, Mrufani alidai kuwa NHIF ilikiuka utaratibu wa kisheria kwa kutumia kigezo kipya wakati wa tathmini kwa kuhitaji nyaraka kama taarifa za benki au barua za mikopo, jambo ambalo halikuainishwa kwenye nyaraka za zabuni. Kwa mtazamo wake, hatua hiyo ilikuwa ni kinyume na kanuni za uwazi na haki katika michakato ya zabuni za umma.

Sambamba na hilo, Mrufani alipinga uamuzi wa NHIF kukusudia kumpa zabuni mzabuni aliyependekezwa kupewa tuzo, akidai kuwa zabuni yake ilikuwa na gharama nafuu zaidi na hivyo ingeisaidia serikali kuepuka kuingia gharama za ziada zinazofikia TZS 46,000,000 fedha ambazo zingeweza kutumika kwenye shughuli nyingine za maendeleo.

Kwa upande wake, NHIF ilieleza kuwa kigezo cha uwezo wa kifedha kilikuwa wazi na kilihitaji uthibitisho wa upatikanaji wa rasilimali fedha, ambapo Mrufani aliwasilisha barua yake binafsi isiyoambatana na vielelezo vya kuthibitisha madai yake, kama vile taarifa za benki, barua za mikopo, au dhamana za kifedha kutoka taasisi zinazotambulika. NHIF ilisisitiza kuwa wazabuni wengine waliweza kukidhi kigezo hicho ikiwemo mzabuni aliyependekezwa kupewa tuzo ambaye aliwasilisha barua kutoka benki ya Tanzania Commercial Bank (TCB) hivyo kufanya mchakato wa tathmini kuwa wa haki na unaozingatia usawa.

Kuhusu hoja ya Mrufani kuwa NHIF alitumia vigezo vipya wakati wa tathmini, NHIF ilikanusha madai hayo na kufafanua kuwa kigezo hiko kiliorodheshwa wazi kwenye nyaraka ya zabuni katika Tamko la Mahitaji (Statement of Requirements) hivyo tathmini ya zabuni ilifanyika kwa kuzingatia kikamilifu vigezo vilivyowekwa kwenye nyaraka za zabuni.

Aidha, NHIF ilieleza iwapo Mrufani aliona kuwa kigezo cha upatikanaji wa rasilimali fedha hakikuwa wazi, alipaswa kuomba ufafanuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma kabla ya tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni. Kwa kuwa hakufanya hivyo, ilimaanisha kuwa alielewa na kukubaliana na masharti hayo. Hivyo, NHIF iliomba rufaa hiyo itupiliwe mbali kwa kukosa mashiko.



Katika kujibu hoja bishaniwa kuhusu uhalali wa Mrufani kuenguliwa kwenye mchakato wa zabuni, PPAA ilichambua kwa kina nyaraka zilizowasilishwa na Mrufani kupitia mfumo wa Kieletroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) katika kipengele cha uwezo na upatikanaji wa kifedha na kubaini kuwa Mrufani aliambatisha barua ambayo haikutosheleza kuthibitisha madai yake, kwani licha ya kueleza namna fedha zingepatikana, hakukuwa na ushahidi wa kuaminika kutoka kwa taasisi za kifedha au wateja waliothibitisha uwepo halisi wa fedha hizo.

Aidha, PPAA ilichambua madai ya Mrufani kuwa NHIF ilitumia vigezo vipya vya tathmini ambavyo havikuwepo kwenye nyaraka za zabuni. Baada ya kupitia ripoti ya tathmini, ilibaini mchakato wa tathmini ulifanyika kwa kuzingatia kikamilifu vigezo vilivyowekwa kwenye nyaraka za zabuni na hakuna kigezo kipya kilichowekwa wakati wa tathmini, kinyume na madai ya Mrufani. Hivyo, PPAA ilitupilia mbali hoja hiyo.

Kuhusu madai ya Mrufani ya kwamba Mzabuni aliyependekezwa aliwasilisha bei ya juu zaidi kuliko yake, PPAA ilibaini kuwa madai haya hayana mashiko kwani Sheria ya Ununuzi wa Umma inataka mzabuni mshindi kuwa kwa mzabuni mwenye zabuni iliyotathminiwa kuwa chini (Lowest Evaluated Tenderer) na si kwa yule aliyewasilisha bei ya chini tu. Kwa kuwa Mrufani aliondolewa katika hatua ya tathmini ya kibiashara (Commercial Evaluation Stage) zabuni yake isingeweza kuendelea katika hatua nyingine za tathmini, ikiwemo ulinganisho wa bei. Hivyo basi, hoja hiyo ilionekana kutokuwa na mashiko kisheria.

Kutokana na uchambuzi wa hoja zilizotajwa hapo juu, PPAA ilitupilia mbali rufaa hii kwa kukosa mashiko na kuamuru NHIF kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia Sheria, hakuna gharama zozote za shauri zilizotolewa.

# PPAA YATUPILIA MBALI RUFAA DHIDI YA TAMISEMI

## Yaamuru Tamisemi kuendelea na mchakato wa Zabuni kwa kuzingatia sheria

**Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetupilia mbali rufaa iliyowasilishwa na M/S Anhui Zhenwei Construction Co. Limited (Mrufani) dhidi ya Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) (Mjibu Rufaa) kwa kukosa mashiko, na kuiruhusu TAMISEMI kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia sheria.**

Uamuzi huo ulitolewa tarehe 22 Januari 2026 mbele ya Jaji mstaafu Mh. Awadh Bawazir, kufuatia rufaa hiyo inayohusiana na zabuni ya ujenzi wa Bohari ya Mabasi yaendayo Haraka (BRT) katika eneo la Ubungo Maziwa pamoja na ubomoaji wa bohari iliyopo maeneo ya Jangwani jijini Dar es Salaam.

Rufaa ya Mrufani ilitokana na kutoridhishwa na uamuzi wa TAMISEMI katika malalamiko aliyoyawasilisha baada ya zabuni yake kuenguliwa kwenye mchakato wa ununuzi wa umma kutokana na kutokidhi vigezo vya kuonyesha uwezo wa upatikanaji wa rasilimali za kifedha, na kutokusaini ipasavyo Tamko la Utendaji kuhusu Unyanyasaji wa Kijinsia (SEA).

Aidha, Mrufani aliwasilisha vyeti vitatu vya mikopo ya benki kutoka benki mbili ambavyo vilikuwa vimepitwa na muda, havikuelekezwa kwa mlalamikiwa na havikuainisha jina au namba ya mradi. Vilevile, fomu ya SEA ilisainiwa na mtu ambaye hakuwa na mamlaka ya kufanya hivyo.

Hata hivyo, Mrufani alikata rufaa akidai kuwa mchakato wa zabuni haukufuata Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake zinazosisitiza uwazi, ushindani, uadilifu na thamani ya fedha. Alieleza kuwa TAMISEMI ilikiuka misingi hiyo katika zabuni husika.



Wakati wa usikilizwaji wa shauri hilo, Mrufani alieleza kuwa nyaraka ya zabuni ilikuwa na kigezo kilichowataka wazabuni kuonesha uwezo wa kupata fedha kiasi cha TZS 9,328,000,000. Ili kukidhi sharti hilo, alieleza kwamba yeye aliambatanisha vyeti vitatu vya mikopo ya benki kutoka Bank of China kikimpa mkopo wa Yuan milioni 90, Industrial Bank Co. Ltd kikitoa ukomo wa mkopo wa Yuan milioni 50 na cha tatu kutoka benki hiyo hiyo kikithibitisha salio la akaunti la RMB 30,000,000. Aliendelea kueleza kuwa fedha hizo zikibadilishwa kuwa Dola za Marekani (USD), zinakuwa sawa na Dola milioni 17, kiwango ambacho kinazidi sharti la TZS 9,328,000,000 lililoainishwa kwenye nyaraka ya zabuni. Hivyo, alisisitiza kuwa alikidhi kigezo cha kuonyesha upatikanaji wa rasilimali za kifedha. Na alisisitiza kuwa vyeti vyake vilitolewa kwa wakati unaotakiwa, hivyo vilikidhi matakwa ya zabuni.

Mrufani alidai kuwa nyaraka ya zabuni haikuweka masharti ya muundo maalum wa vyeti vya mikopo, hivyo alikuwa huru kuwasilisha vyeti vyovyote vinavyoonesha uwezo wa kifedha.

Alisema TAMISEMI haikuwa sahihi kuiondoa zabuni yake kwa hoja kuwa vyeti hivyo havikuwa na jina lake, la mradi au namba ya zabuni.

Pia aliwasilisha hoja kwamba TAMISEMI ilipuuza maelekezo kwa Wazabuni ambayo yanaruhusu kuomba ufafanuzi kutoka kwa wazabuni wakati wa tathmini. Badala ya kuomba ufafanuzi kuhusu vyeti vya mikopo, TAMISEMI iliendelea kuiondoa zabuni ya Mrufani bila kufanya juhudi ya kupata ufafanuzi huo.

Mrufani alidai kuwa vyeti vipya vya mikopo vilivyowasilishwa wakati wa mapitio ya kiutawala vilikuwa ni ufafanuzi wa nyaraka za awali, si mbadala wake. Alisisitiza kuwa TAMISEMI ilikosea kuvichukulia kama nyaraka mpya badala ya ufafanuzi wa taarifa zilizokuwepo.

Mrufani alidai kuwa nyaraka ya zabuni na sampuli ya fomu ya SEA kwenye NeST hazikuhitaji saini ya mkono wala kusainiwa na mwenye Hati ya uwakala. Hata hivyo, baada ya kuoneshwa sampuli ya fomu na Mamlaka ya Rufani, alikiri kutokukidhi sharti hilo.


Mrufani alidai kuwa zabuni yake ilikuwa na punguzo la 4.5%, bora zaidi kuliko 4% ya Mzabuni Mshindi. Alisema TAMISEMI iliiondoa zabuni yake kwa dhana za kibinafsi kuhusu vyeti vya mikopo badala ya kuzingatia ofa hiyo na hivyo kumpa zabuni Mzabuni Mshindi kunasababisha upotevu wa takribani asilimia 8.5 ya thamani ya mkataba, sawa na TZS bilioni 3.4 ya fedha za walipa kodi ambazo zingeweza kuelekezwa kwenye miradi mingine ya maendeleo.

Kwa upande wake, TAMISEMI ilieleza kuwa zabuni

ya Mrufani iliondolewa katika hatua ya tathmini kwa kushindwa kukidhi kigezo cha kuonyesha upatikanaji wa rasilimali fedha wa kiasi cha TZS 9,328,000,000. Iliongeza kuwa Mrufani aliwasilisha vyeti vitatu vya mikopo kutoka benki ya Agricultural Bank of China kikitoa mkopo wa Yuan (CNY) milioni 90; Industrial Bank Co. Ltd (tawi la Hefei) kikitoa mkopo wa Yuan milioni 50; na cha tatu pia kilitolewa na Industrial Bank Co. Ltd (Hefei Economic and Technological Development Zone, Science and Technology Sub-branch) kikithibitisha salio la akaunti ya RMB 30,000,000.

Aidha, TAMISEMI ilieleza kuwa wakati wa tathmini, kamati ya tathmini ilibaini kasoro zikiwemo, cheti cha kwanza kilichotoa mkopo wa Yuan milioni 90 kutokuelekezwa kwa taasisi nunuzi, wala kuwa na jina la mradi au namba ya zabuni. Pia hakikuwa na namba ya rejea, taarifa muhimu za benki husika, wala anuani mahsusi ambazo zingeonyesha kama kilikuwa mahsusi kwa mradi unaolalamikiwa na pia hata kuiwezesha kufanya uhakiki.

Aidha, ilieleza kuwa cheti cha pili cha mkopo kilichoonesha kiasi cha Yuan milioni 50 kilikuwa na kasoro zinazofanana ikiwemo tahadhari (disclaimer) iliyoeleza kuwa si barua ya dhamana wala ahadi. Kauli ambayo ilionesha benki haikutoa uhakika wa upatikanaji wa mkopo huo na hivyo Mrufani hangeweza kutegemea kama dhamana ya kifedha kwake.



Kuhusu cheti cha tatu, ilibainisha kuwa nacho kilikuwa na kasoro zinazofanana na cheti cha kwanza, na zaidi ya hapo kilielekezwa kwa Wakala wa Barabara wa Jamhuri ya Malawi, jambo lililokifanya kisiwe na uhusiano na zabuni inayolalamikiwa.

Pia ilielezwa kuwa vyeti vyote vitatu vya mikopo ya benki viliandikwa kwa lugha ya Kichina na baadaye kutafsiriwa kwa Kiingereza lakini tafsiri hazikuwa na mihuri rasmi wala anuani ya taasisi halali ya tafsiri, hivyo kuibua shaka kuhusu uhalali wa tafsiri hizo.

Kuhusu hoja ya Mrufani kuwa nyaraka ya zabuni haikubainisha muundo wa vyeti vya mikopo, TAMISEMI ilirejea Maelekezo kwa Wazabuni (Instructions to Tenderers) yanayowataka wazabuni kuhakikisha uadilifu, ukamilifu na uhalisia wa zabuni zao kabla ya kuziwasilisha kwa taasisi nunuzi. Kinyume na hilo, Mrufani aliwasilisha vyeti viwili vilivyoelekezwa kwake mwenyewe na kimoja kwa Wakala wa Barabara wa Jamhuri ya Malawi.

Kuhusu vyeti vilivyoboreshwa na kuwasilishwa wakati wa maombi ya mapitio ya kiutawala, ilielezwa kuwa maelekezo kwa Wazabuni yanakataza kufanya marekebisho ya zabuni baada ya muda wa mwisho wa uwasilishaji wa zabuni. Na kuhusu kutokukidhi sharti la SEA, TAMISEMI haikuwasilisha lolote kwa kuwa Mrufani alikiri mwenyewe kutokukidhi sharti hilo.

PPAA ilibaini kuwa cheti cha mkopo kutoka Agricultural Bank of China kilikuwa na ukomo wa Yuan milioni 90 lakini muda wake uliisha tarehe 25 Septemba 2025, kabla ya mwisho wa uwasilishaji wa zabuni (20 Oktoba 2025). Aidha, cheti hicho hakikuelekezwa kwa TAMISEMI wala hakikuwa na jina au namba ya zabuni. PPAA ilibaini kuwa kutokana na muda wa mkopo kuisha, hakukuwa na uthibitisho halali wa upatikanaji wa fedha kupitia cheti hicho. Pia, kwa kuwa hakikutaja jina au namba ya zabuni, haikuwezekana kuthibitisha kuwa mkopo ulikusudiwa kwa zabuni husika.

Kuhusu cheti cha pili, kilichotolewa na Industrial Bank Co. Ltd (tawi la Hefei) ambacho kilionekana kuelekezwa kwa Mrufani, kikitoa ukomo wa mkopo wa Yuan milioni 50. Benki haikutoa ahadi wala dhamana ya upatikanaji wa kiasi hicho cha mkopo. Hivyo, hakukuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha hizo. Aidha, sawa na cheti cha kwanza, cheti hiki hakikuainisha jina au namba ya mradi unaohusika.

PPAA ilibaini kuwa cheti cha tatu kutoka Industrial Bank Co. Ltd. kilielekezwa kwa Wakala wa Barabara wa Malawi na kilithibitisha salio la RMB 30,000,000, huku kikiwa na tahadhari sawa na cheti cha pili. Baada ya uchambuzi, PPAA ilihitimisha kuwa cheti hicho hakikuwa na uhusiano na zabuni husika kwa kuwa kilielekezwa kwa taasisi tofauti.

Kuhusu hoja ya Mrufani kwamba nyaraka ya zabuni haikubainisha muundo maalum wa kuonesha upatikanaji wa rasilimali za kifedha, PPAA ilieleza lengo la kigezo hicho ni kuipa taasisi nunuzi uhakika kuwa mzabuni ana mtiririko wa fedha wa kutosha kugharamia utekelezaji wa mradi.

Hivyo, vyeti vya mikopo au barua za uthibitisho wa kifedha vinapaswa kuelekezwa kwa taasisi nunuzi, na vinapaswa kubainisha wazi jina la mradi husika pamoja na namba ya zabuni. Hii huiwezesha taasisi nunuzi kuthibitisha upatikanaji wa fedha hizo. Cheti cha mkopo kinachoelekezwa kwa mzabuni pekee, kama ilivyokuwa kwa Mrufani, hakiwezi kutoa uhakika wa upatikanaji wa fedha, kwani kinaweza kutumika kama ahadi ya fedha kwa miradi mingi kwa wakati mmoja. Aidha, PPAA ilibainisha kuwa vyeti vyote vya mikopo vilivyowasilishwa na Mrufani havikukidhi masharti ya zabuni.

Kwa mujibu wa ripoti ya tathmini, zabuni ya Mrufani haikufika hatua ya tathmini ya kifedha ambapo bei na punguzo lake lingelinganishwa na za wengine. Hivyo, madai yake hayana mashiko.

Kwa msingi huo, PPAA ilitupilia mbali rufaa hiyo bila gharama kwa kukosa mashiko, na kuiruhusu TAMISEMI kuendelea na mchakato wa zabuni kwa kuzingatia sheria.

# Wazabuni Kilwa, Lindi na Mtwara Wapatiwa Mafunzo Juu ya Matumizi ya Moduli ya Uwasilishaji na Ushughulikiaji Rufaa katika Mfumo wa NeST



*Mkuu wa Sehemu ya Rufaa wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Violet Limilabo akiwalisha wasilisho kuhusu uwasilishaji wa malalamiko na rufaa katika Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa taasisi nunuzi mkoani Mtwara hivi karibuni.*

**KATIKA jitihada za kuongeza uelewa wa matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi ya Umma (NeST), Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) imetoa mafunzo kwa wazabuni, wajasiriamali na watumishi wa umma waliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, mikoa ya Lindi na Mtwara.**

Akielezea kuhusu mafunzo hayo ya siku tano kuanzia tarehe 16 hadi 20 Februari, 2026, Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Sheria wa PPAA, Bi. Florida Mapunda amesema kuwa mafunzo hayo yamelenga kutoa elimu kwa wadau wa ununuzi wa umma kuhusu taratibu za uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Ununuzi wa Umma.

"Sheria ya Ununuzi wa Umma imeweka sharti la lazima kwa ununuzi wa umma kufanyika katika mfumo wa NeST. Kutokana na sharti hilo, PPAA kwa kushirikiana na PPRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma) tumejenga moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko katika mfumo wa NeST ili kuwasaidia wadau wa ununuzi wa umma (wazabuni na taasisi za umma) kuwasilisha malalamiko na rufaa kieletroniki," amesema Bi. Mapunda.

Pamoja na mambo mengine, Bi. Mapunda ameongeza kuwa Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST ina manufaa makubwa kwa wazabuni kwani inarahisisha uwasilishaji wa malalamiko ya zabuni kwa njia ya mtandao bila kufika ofisini, jambo linalochangia kuokoa muda, gharama na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma.

Kwa upande wake Mkuu wa Sehemu ya Rufaa wa PPAA, Bi. Violet Limilabo ameeleza kuwa PPAA ina mchango mkubwa katika kulinda haki za wazabuni kwa kuwapa fursa ya kusikilizwa wanapoona hawakutendewa haki katika michakato ya ununuzi wa umma.

Aidha, PPAA imeendelea kuimarisha uwazi na usawa kwa kuhakikisha taratibu za ununuzi wa umma zinafuatwa kwa mujibu wa sheria na kupunguza migogoro kwa kutoa suluhisho la kisheria.

Naye Afisa Ununuzi wa PPRA Kanda ya Kusini, Bw. Aziz Njovu akitoa mafunzo kuhusu moduli mpya za majadiliano (negotiations) na uandaaji, upekuzi na utiaji saini wa Mkataba (Contract preparation, vetting and signing) kwenye mfumo wa NeST, alisema kwa sasa mchakato wa majadiliano na utiaji saini wa mkataba unahitimishwa kwa njia ya mtandao.

"Matumizi ya mfumo wa NeST yameendelea kuimarisha uwajibikaji na kurahisisha ufuatiliaji wa mikataba ya ununuzio wa umma," amesema Bw. Njovu.

Mafunzo hayo yamewahusisha washiriki 322 ambao ni wataalamu wa sheria, Tehama na ununuzi pamoja na wazabuni, makundi maalum yakiwemo wanawake, vijana, wazee na watu wenye mahitaji maalum pamoja na mafundi wa ndani.

Mafunzo kuhusu matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika mfumo wa NeST yaligawanyika katika makundi matatu ambapo Kundi la kwanza ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa tarehe 16 Februari, 2026, Mkoa wa Lindi tarehe 17 na 18 Februari, 2026 na Mkoa wa Mtwara tarehe 19 na 20 Februari, 2026.

Mafunzo hayo ni mwendelezo wa mafunzo ya awali yaliyofanyika katika Kanda ya Pwani, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati.

# HABARI PICHA



*Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando akizungumza na Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea wakati PPAA ilipofanya mafunzo kwa wadau wa ununuzi wa umma katika ofisi za halmashauri hiyo hivi karibuni. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, Wakili. Bashir Muhoja.*



*Afisa Sheria wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. Venance Mkonongo akiwasilisha mada kuhusu uwasilishaji na ushughulikiaji wa malalamiko na rufaa katika ununuzi wa umma kwa wazabuni na taasisi nunuzi walioshiriki mafunzo mkoani Ruvuma hivi karibuni.*



*Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Jenerali Ahmed Abbas Ahmed akimsikiliza Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando wakati Bw. Sando alipomtembelea ofisini kwake wilayani Songea mkoani Ruvuma, Machi, 2026. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Fedha wa PPAA, Bw. Aliko Mwaiteleke.*

PUBLIC PROCUREMENT APPEALS AUTHORITY
Efficient and Fair Appeals Dispensation
PPAA
MAMLAKA YA RUFANI YA ZABUNI ZA UMMA
BULLETIN
UTOAJI RUFAA KWA UFANISI NA HAKI
PPAA
Toleo Na: 08 Januari - Machi 2026

# HABARIPICHA

*Ujumbe wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA) ukiongozwa na Meneja wa Usimamizi wa Rufaa na Sheria, Bi. Florida Mapunda (aliyekaa katikati) ukiwa na washiriki wa mafunzo kuhusu Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kwenye mfumo wa NeST kwa wazabuni na taasisi nunuzi wa Mkoa wa Mtwara.*





*Mkuu wa Sehemu ya Sheria ya Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bi. Agnes Sayi akiwasilisha mada kwa washiriki walioshiriki mafunzo kuhusu Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa kwenye mfumo wa NeST kwa wazabuni na taasisi nunuzi wa mikoa ya Iringa na Njombe.*

*Kaimu Kamishna wa Sera za Ununuzi wa Umma, Bw. Alex Haraba (kulia), pamoja na Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando wakishiriki mahojiano katika kipindi cha Pevuka kinachorushwa na Radio U-FM Jijini Dar es Salaam. Viongozi hao walipata fursa ya kuelimisha Umma kuhusu umuhimu wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025. Sera hiyo inatarajiwa kuzinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 8 Aprili 2026 Jijini Dodoma.*

